HALMASHAURI YA WILAYA YA TUNDURU.

SHULE YA SEKONDARI NAMWINYU,
S.L.P 433,
TUNDURU.
14/12/2020

MKOA WA RUVUMA

SIMU Na:(Mkuu wa shule) 0769 495 567
0783 519 610

(M/M/Shule) 0755233924

0687199607

MZAZI/MLEZI WA .....
S.L.P .....
TUNDURU.

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

1. **UTANGULIZI**
   - Nafurahi kukujulisha ya kwamba mwanao..... amechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari **NAMWINYU** iliyopo kata ya Namwinyu, tarafa ya Matemanga, wilayani Tunduru.
   - Shule hii ni ya kutwa (Day school)
   - Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 saa moja na nusu (1:30) asubuhi kwa muhula wa kwanza. Unatakiwa umlete mwanao siku tajwa bila kukosa.
   - Mzazi/mlezi unatakiwa umwandalie mahitaji yake mapema ili aweze kuwahi masomo

2. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**
   - **SARE ZA SHULE**

     A. WAVULANA
     - Suruali mbili za kitambaa cha rangi ya **kijivu iliyopauka** (Light grey)
     - Mashati 2 meupe mikono mifupi (Lisilo bana)
     - Viatu vya **ngozi, vyeusi, vya** kufunga na kamba jozi mbili.
     - Mkanda **mweusi** wenye upana wa inchi 1.
     - Soksi ndefu nyeupe jozi tatu (03)
     - Sweta rangi ya **kijivu iliyopauka** (Light grey) lenye shingo ya V.

     B. WASICHANA
     - Sketi 2 za kitambaa cha rangi ya **kijivu iliyopauka** (Light grey)
     - Mashati 2 meupe mikono mifupi (Lisilo bana)**AU**
     - Hijabu kwa atayependa (Sio mtandio) ivaliwe pamoja na shati jeupe la nusu kanzu la mikono mirefu
     - Viatu vya **ngozi, vyeusi, vya kufunga na kamba** jozi mbili.
     - Soksi ndefu nyeupe jozi tatu (03)
     - Sweta rangi ya **kijivu iliyopauka** (Light grey) lenye shingo ya V.

C. **NGUO ZA KAZI NA MICHEZO.**

- **WAVULANA**: Suruali nyeusi, T-Shirt ya bluu, bukta ya bluu, raba jozi 1,
- **WASICHANA**: Sketi nyeusi, T-Shirt ya bluu, Traki suti ya bluu, raba jozi 1

3. **VIFAA VYA KUJIFUNZIA.**
   - Daftari kubwa09 (counter book quire 2 au zaidi)
   - Daftari ndogo za kawaida (Kwa mfano "msomi")kwa ajili ya mazoezi kila somo.
   - Kalamu (za wino na za risasi), rula na mkebe wa hesabu (Mathematical set)
   - Kamusi ya kujifunzia kiingereza (English – Swahili dictionary) ni muhimu kwa ajili ya kujifunzia

4. **VIFAA VYA USAFI NA KAZI**
   - Ndoo ndogo ya lita 10 kwa wote
   - Fagio **laini za dukani** (soft broom) kwa wote
   - Jembe kubwa mpya lenye mpini **(Kwa wavulana pekee)**
   - Fyekeo mpya **(Kwa wasichana pekee)**

5. **MCHANGANUO WA MCHANGO WA CHAKULA**

NA	CHAKULA/MCHANGO	MUHULA	MWAKA
1	MAHINDI	Debe 2 (Kilo 40)	Debe 4 (Kilo 80)
2	MBOGA	Kilo 12	Kilo 24
3	CHUMVI	Kilo 1	Kilo 2
4	MAFUTA	Lita 1	Lita 2
5	MPISHI	Tsh 5,000/=	Tsh 10,000/=
6	KUSAGA	Tsh 4,000/=	Tsh 8,000/=

MUHIMU:

- Mchango wa chakula ni lazima kwa kila mwanafunzi anayejiunga Namwinyu sekondari.
- Michango ya chakula itapokelewa kuanzia kiwango cha robo mwaka, kwa mfano: mahindi debe moja, mboga kilo 6, kusaga 2000/= mpishi Tsh 5000/= mafuta lita 1, chumvi kilo 1.
- Mboga za nafaka zote zinapokelewa isipokuwa mbaazi hazitapokelewa (Hii ni kwa mujibu wa makubaliano yaliyofanyika kwenye kikao cha wazazi)
- Shule ina uhaba mkubwa wa viti na meza, mzazi anashauriwa kumnunulia mwanawe angalau kiti cha plastiki ambacho kitakua mali ya mwanafunzi na pale ambapo shule itakua na viti vya kutosha atarudi nacho nyumbani.
- Ili kuwa na uhakika wa matibabu ya mwanafunzi endapo ataumwa, unatakiwa umkatie bima mpya ya matibabu mwanao au aje na pesa Tsh 5000/= ili akatiwe bima ya matibabu

6. **VIFAA VINGINE.**
   - Kila mwanafunzi aje na picha ya paspoti ambayo amepiga hivi karibuni akiwa amevaa sare ya shule.
   - Kila mwanafunzi awe na vifaa vyake vya kulia chakula kama vile sahani, bakuli, kikombe na kijiko. Ni muhimu sana.

7. **TAFADHARI TEKELEZA YAFUATAYO KABLA YA KUJA SHULENI.**
   - ❖ Soma kwa umakini sharia za shule zilizoambatanishwa pamoja na maelekezo haya
   - ❖ Hakikisha umepima afya yako katika hospitali ya serikali na daktari ajaze fomu ya vipimo iliyoambatanishwa na maelekezo haya
   - ❖ Hakikisha umepata mahitaji na vifaa vyote muhimu kwa ajili ya kujifunzia
   - ❖ Ufikapo shuleni ripoti ofisi ya **MakamuMkuu wa shule** ili usajiliwe na si vinginevyo.
8. Pamoja na maelekezo haya, tunaambatanisha viambatanisho vifuatavyo ambavyo mzazi/mwanafunzi atalazimika kuvijaza na kuvitekeleza.
   a) Kiambata A, sheria za shule. Azisome na kuzielewa
   b) Kiambata B, ijazwe na mzazi/mlezi na pia mwanafunzi ajaze sehemu yake.
   c) Kiambata C, kwa ajili ya vipimo vya afya (Hospitalini). Mwanafunzi apimwe kabla ya kuripoti shuleni.

Nakutakia maandalizi mema tayari kwa kujiunga na shule hii.

MOTTO WA SHULE.
ELIMU BORA KWA WOTE (QUALITY EDUCATION FOR ALL)
AHSANTE

MZIWANDA J.N
MKUU WA SHULE.
(0783519610/0769495567)

MKUU WA SHULE
NAMWIIYU SEKONDARI
S. L. P. 433 TUNDURU

KIAMBATA A: SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kanunu zake na kama ilivyorekebishwa kwa sharia Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote kwa maandishi na serikali kupitia wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Mwanafunzi atatakiwa kuzifuata sharia hizi kikamilifu.

1. MWANAFUNZI.
    a) Sharti asimame na kuwasalimia kwa adabu walimu na mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita mahali alipo mwanafunzi.
    b) Kuwapokea walimu/wageni wanaoingia shuleni.
    c) Wasitumie lugha mbaya wakati kati yao wenyewe, kwa walimu na kwa watu wengine.
    d) Wawaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kama wazazi wao. Uhusiano wa wanafunzi kwa walimu wao ni wa mtoto na baba au mama yake.
    e) Washirikiane, wapendane na kusaidiana wao wenyewe katika mambo mbalimbali ya masomo na wathamini na kuziheshimu kazi za aina zote.
    f) Wathamini muda na kuwahi katika shughuli zote za shule zilizopo katika ratiba ya kila siku. Kila mmoja awahi na ahudhurie wito wa dharura (emergence), waitikie wito au ishara ya kuwaita bila kuchelewa.
    g) Wathamini na kuziheshimu mali binafsi na mali za umma.
    h) Waheshimu bendera ya Taifa, picha ya viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
    i) Wanapokuwa darasani, kwenye mikutano nk wanyooshe mikono juu na kusimama wanapouliza na kujibu swali.
    j) Wakae kimya wanapokuwa darasani. Wasitoke nje bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.
    k) Waoneshe mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote.
    l) Wanafunzi watatakiwa kuwa safi kimwili na kimavazi. Mavazi ya kihuni hayatakiwi hapa shuleni.

2. **Ni marufuku**
    i. Kuvuta sigara ya aina yoyote
    ii. Kutumia madawa ya kulevya
    iii. Kushiriki aina yoyote ya ulevi.
    iv. Kufuga kucha ndefu, ndevu, nywele, kuweka dawa nywele, kusuka, kunyoa mtindo usiotakiwa kama kiduku, kipara na mitindo mingine, kupaka hina, wanja na kunyoa nyusi.
    v. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima.
    vi. Kuzurura hovyo.
    vii. Kugombana na mwenzake au mtu yeyote, matusi na uonevu wa aina yoyote.

    Kutembelea sehemu zifuatazo ni marufukua isipokua kwa kibali maalumu:-
        I. Chumba cha mwalimu/walimu na ofisi zake.
        II. Jikoni

III. Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio waalimu.

Ni marufuku kuto hudhuria:-

- Vipindi vya masomo ndani nan je ya darasa.
- Michezo na kazi zote za mikono
- Baraza la shule, kupandisha bendera ya Taifa, ukaguzi wa usafi n.k

Ni mwiko kabisa kwenda au kuonekana katika sehemu zifuatazo:-

i. Vilabu vya pombe na baa

ii. Majumba ya starehe

iii. Majumba ya kufikia na kulala wageni (Guest House)

3. Wanafunzi wote wawahi kwenye shughuli zote za shule kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya kila siku ya shule.
4. Sare ya shule

A. Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa kwenye maelekezo ya kujiunga na shule hii. Hivyo kila mwanafunzi ni SHARTI avae sare ya shule iliyo safi na nadhifu wakati wote.

- Wa masomo darasani.
- Anapofika shule kwa sababu yoyote muda wa masomo.
- Anapotoka nje ya shule kwa shughuli za kishule.
- Wa mhadhara wa shule(Baraza la shule)
- Anapokwenda hospitali.
- Wa maandamano(Yanakubalika na kuruhusiwa na mamlaka husika)

B. Sare ya shule isivaliwe pamoja na vitu vifuatavyo:-

Kofia, herein, bangili, viatu vya ghorofa, pete na vibanio vya nywele.

5. Yafuatayo ni makossa mara baada ya kuthibitishwa yanaweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule mara moja

a) Wizi
b) Uasherati, ubakaji na ushoga/usagaji.
c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
d) Makossa ya jinai.
e) Kupiga au kupigana.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuoa au kuolewa.
i) Kupata mimba au kusababisha mimba nje au ndani ya shule.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga Amani na usalama wa watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.

TANBIHI:

Mwanafunzi atapata msamaha wa kutofanya kazi iwapo ana cheti cha Daktari kinachothibitisha asifanye kazi.

KIAMBATA C: MEDICAL EXAMINATION FORM.

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE, TECHNOLOGY AND VOCATION TRAINING.

TUNDURU DISTRICT COUNCIL.

NAMWINYU SEC. SCHOOL,

S.L.P 433,

TUNDURU.

DATE_____

MEDICAL OFFICER

……

……

……

REF: MEDICAL EXAMINATION FOR THE SELECTED STUDENTS 2020.

The title above is concerned.

Kindly check the selected students to join for secondary education in my school so as to verify his/her fitness to continue with his/her studies and state some of the health recommendations that need special attention.

Please examine and fill the following: -

1. Student's full name_____
2. Age _____ Sex _____
3. Blood count (Red and white) _____
4. Stool examination _____
5. Urinalysis _____
6. Syphilis _____
7. Venereal Disease Test _____
8. T.B Test _____
9. Eye test _____
10. Ear test _____
11. Chest _____
12. Spleen _____
13. Abdomen _____
14. Urine for pregnancy test _____

Additional information (If any) eg Physical defects or impairment (s) ie arm, leg, chronic disease etc.

_____

_____

_____

I certify that the above is fit/unfit to pursue education as stated above

_____	_____	_____	_____
Signature	Designation	Station	Date